



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA



Tarehe 30/09/2024

*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb. Na. LDC/D.60/46VOL.IV /58

# TANGAZO

**KWA UMMA WILAYANI LUDEWA KUHUSU KUFUNGULIWA KWA  
UTOAJI WA MIKOPO KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA  
WATU WENYE ULEMAVU.**

(Limetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 7 (1) ya utoaji na usimamizi wa mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu za mwaka 2024.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa anatangaza kufunguliwa kwa mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu na uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ambapo jumla ya Shilingi 491,184,163 zimetengwa katika robo ya 1 ya mwaka wa fedha. 2024/2025. Hivyo, Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi kwa njia ya mfumo katika Ofisi za serikali za Mitaa (**Kijiji/Kata**) zilizopo katika maeneo yenu.

---

Barua zote zitumwe kuitilia anuanī ifuatayo:-

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, 3 Barabara ya Bomani, S. L. P 19, **59401 NJOMBE**,  
Simu +255 26 2790120, Nukushi + 255 26 2790128, Baruapepe; [ded@ludewadc.go.tz](mailto:ded@ludewadc.go.tz), Tovuti [www.ludewadc.go.tz](http://www.ludewadc.go.tz)

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo: -

- (i) Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenyе ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na Halmashauri kwa njia ya mfumo wa kieletroniki.
- (ii) Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali,
- (iii) Kikundi cha Wanawake na Vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha watu wenyе ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6 a(1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenyе ulemavu endapo timu ya menejimenti ya halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine,
- (iv) Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali; na
- (v) Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenyе akili timamu na wenyе umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa kuwa na wanakikundi wenyе umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

Maombi yote yatumwe kuititia mfumo wa kielekroniki (**tembelea tovuti: mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz**) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata husika au Mtendaji wa Kata husika.

---

Barua zote zitumwe kuititia anuani ifuatayo:-


Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, 3 Barabara ya Bomani, S. L. P 19, **59401 NJOMBE**,  
Simu +255 26 2790120, Nukushi + 255 26 2790128, Baruapepe: [ded@ludewadc.go.tz](mailto:ded@ludewadc.go.tz), Tovuti [www.ludewadc.go.tz](http://www.ludewadc.go.tz)

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo; Barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa mtendaji wa kijiji/mtaa kwa kuandika jina lake, saini na kugonga mhuri wa serikali ya Kijiji, Muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo, andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyio ndani ya mfumo wa kieletroniki na taarifa ya akaunti ya benki yenyeye jina la kikundi au Jina la mtu mwenye ulemavu mmoja aliyekosa wenzake wa kuungana nao

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 15 mwezi 10 mwaka 2024

**Tangazo hili limetolewa na: -**

  
Sunday Deogratius  
Mkurugenzi Mtendaji(W)  
**HALMASHAURI YA LUDEWA**



---

Barua zote zitumwe kupitia anuanzi ifuatayo:-

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, 3 Barabara ya Bomani, S. L. P 19, 59401 NJOMBE,  
Simu +255 26 2790120, Nukushi + 255 26 2790128, Baruaapepe: [ded@ludewadc.go.tz](mailto:ded@ludewadc.go.tz), Tovuti [www.ludewadc.go.tz](http://www.ludewadc.go.tz)